BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 02 Juni, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2025/2026.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

60. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Kuna Kada ambazo wafanyakazi huzisomea na kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi na kuondokana na kufanyakazi kwa mazowea.

    (a) Ni Kada zipi ambazo watumishi wetu hupewa kipaumbele na kuongezewa maslahi zaidi.

(b) Kwa kuwa kada ya Katibu Muhtasi (Secretarty) ni muhimu kama zilivyo kada nyengine kwa wafanyakazi wa Serikali yetu, kwa nini kada hii ina ugumu wa uboreshwaji wa maslahi kama ilivyo kwa kada nyengine.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

122. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Jimbo la Mwanakwerekwe linachukua nafasi muhimu na ya msingi ya kuwa na sehemu ya kuhifadhia miili ya maiti na kuwa pumziko la mwisho kwa maisha ya mwanadamu.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inafikiria kuweka ulinzi wa kutosha katika eneo hili dhidi ya uharibifu unaofanyika kila siku.

(b) Ni kwa kiasi gani Serikali itaweza kuliimarisha eneo hili kuwa nadhifu na la kupendeza kwa kuwa ni kituo cha mwisho kwa kila mtu.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

31. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali katika kufanikisha shughuli zake inatafuta vyanzo mbali mbali vya fedha ikiwemo mikopo katika taasisi za ndani ya nchi. Lengo la mikopo hii ni kuweza kufanikisha kazi ilizojiwekea. Pamoja na jitihada hii kumekuwa na mkanganyiko wa ukubwa wa deni la ndani na fedha ambazo Serikali inadaiwa.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha inayodaiwa Serikali na taasisi za ndani ya nchi tokea 2020.

(b) Je, ni taasisi gani za ndani ambazo Serikali imekopa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

(c) Je, ni kiasi gani cha madeni kimelipwa kwa taasisi hizo za ndani na kwa utaratibu gani.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

298. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Siku nyingi sana zimepita tokea Serikali ilipoyatangaza maeneo ya Fumba, Dunga Zuze na Micheweni kuwa maeneo huru.

(a) Je, ni ipi 'status' iliyofikiwa ya maeneo huru ya Micheweni hadi sasa ukiachilia mbali ule utengenezaji wa barabara.

(b) Je, ni upi mpango wa haraka uliopangwa wa kuyaendeleza maeneo haya.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

70. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zao la karafuu ni sehemu ya uingizaji wa pato la Taifa, lakini uzalishaji wa zao hili unashuka kutokana na kufa kwa miti ya mikarafuu.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea kufa kwa miti ya mikarafuu.

(b) Kuna utafiti wowote wa kitaalamu uliofanywa juu ya tatizo hili.

191. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa vile tuna malengo ya kampeni ya kuifanya Zanzibar kuwa ya kijani.

Je, kuna matayarisho gani ya maandalizi ya kuwa na aina ya miti vivuli itakayopandwa kando kando mwa barabara zetu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

202. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamatuni na Michezo:

Tathmini ya mashindano makubwa ya Quraan yanayoandaliwa na ZBC ipo vipi kwa muktadha mzima.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

228. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kiasi gani taasisi za kielimu na vyuo vikuu mbali mbali binafsi vimeitika na kuimarisha mifumo ya mitaala yao kwa muktadha wa mabadiliko ya Mtaala Mpya.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

231. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Inasemekana katika changamoto inayoikumba Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, ni elimu ndogo kwa mafundi pamoja na uhaba wa mafundi wa magari ya kisasa.

(a) Je, suala hili kwa sasa liko vipi.

(b) Je, kwa kiasi gani Wakala wa Karakana Kuu wanatimiza lengo lao walilojipangia kwa sasa.

(c) Je, suala la Karakana likoje kwa upande wa kisiwani Pemba.

282. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Vitongoji Kibokoni ni miongoni mwa barabara zilizoahidiwa kujengwa kwa muda mrefu sasa.

Je, ni lini ahadi hii itatimizwa.

**Wizara ya Afya:**

287. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Dunia kwa sasa inashuhudia kukatwa kwa misaada kupitia programu nyingi za kiafya ikiwemo ufadhili wa programu za kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na maradhi mengine, hali inayohatarisha maisha ya watu wengi.

Ni upi mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa Serikali kupitia Wizara ya Afya kuweza kufadhili programu hizi na kutorudisha nyuma mafanikio ya kiafya yaliyopatikana.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni mambo gani ya kipekee yanayoifanya Nyumba ya Maajabu kujijengea umaarufu mkubwa katika pembe zote za dunia.

(b) Kwa kiasi gani utafiti wa kina umefanyika kuanzia chini ya jengo hadi kwenye paa baada ya kuondoka kwa tawala ya kifalme ndani ya jengo hili maarufu duniani.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**02 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**